INTERNATIONAL BACCALAUREATE
BACCALAURÉAT INTERNATIONAL
BACHILLERATO INTERNACIONAL



**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHELI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SUAHELI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Monday 8 May 2000 (morning)
Lundi 8 mai 2000 (matin)
Lunes 8 de mayo del 2000 (mañana)

3 hours / 3 heures / 3 horas

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Section A: Write a commentary on one passage. Include in your commentary answers to all the questions set.
- Section B: Answer one essay question. Refer mainly to works studied in Part 3 (Groups of Works); references to other works are permissible but must not form the main body of your answer.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Section A : Écrire un commentaire sur un passage. Votre commentaire doit traiter toutes les questions posées.
- Section B : Traiter un sujet de composition. Se référer principalement aux œuvres étudiées dans la troisième partie (Groupes d'œuvres) ; les références à d'autres œuvres sont permises mais ne doivent pas constituer l'essentiel de la réponse.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Sección A: Escriba un comentario sobre uno de los fragmentos. Debe incluir en su comentario respuestas a todas las preguntas de orientación.
- Sección B: Elija un tema de redacción. Su respuesta debe centrarse principalmente en las obras estudiadas para la Parte 3 (Grupos de obras); se permiten referencias a otras obras siempre que no formen la parte principal de la respuesta.

**SEHEMU A**

*Kifafanue kimoja kati ya vifungu vifwatavyo:*

**1.** (a)

Baada ya miezi, Faki alirudi safarini. Kabla ya siku nyingi hazijapita, ***vibilifitina*** na kina ***pangu pakavu tia mchuzi*** walimweleza Faki kadhia yote iliyokuwa ikipita yeye alipokuwa hayupo. Kwanza Faki asisadiki akaona kuwa ni uwongo Doto hawezi kufanya hivyo kwa mapenzi wanayopendana. Faki aliziba macho na kutia komango masikioni asisikie yanayosemwa. Mapenzi yalimtia upofu na uziwi. Doto alipoona kuwa anapendwa, na Faki hawezi kumkosa, alijasurisha kuwaleta rafikl zake nyumbani kwake na kufanya vitendo vyake kwa dhahiri bila ya kujali au kuogopa.

Mambo yalipokithiri Faki hakuweza kustahamili tena, ila alimwasa na kumwambia ya kuwa vitendo anavyotenda si vyema na vinamchukiza: itakuwa bora akiviacha na akawaepuka marafikl zake. Doto alikuja juu na kula mori kwa maneno hayo, ati kwa kuwa Faki anamtuhumu anafanya vitendo vibaya. Moyo wa kupenda hauna kinyongo, Faki alisunyaa na kunyerereka. Mambo yaliendelea na kutia maji maziwani. Sasa Faki hakuweza kustahamili tena ila alimweleza mkewe vizuri. Doto alilia na kutaka kurejea kwao. Faki alisema kuwa hapana haja ya hayo kwa sasa, lakini itakuwa bora pindi wakikaa nyumba mbili mbalimbali mpaka hasira zao zi’she. Faki alihama akamwamchia nyumba Doto. Baada ya kupita haya makazi yao na mapenzi yao yalikuwa segemnege, na huenda zikapita siku kabla ya nyuso zao hazikuonana. Ingawa Doto alipeleka barua kwao na yeye kuletewa kuelezwa kila kitu, lakini hajawaarifu ya kuwa ana ugomvi na mumewe. Baada ya siku nyingi za kupatikana ugomvi na suitafahamu, Doto alisita kupeleka barua. Haya yaliwatia wahaka watu wake kwani hiyo haikuwa ni desturi yake… Maka’zi ya upweke na kuwa mbali na mtu anayempenda yalimchosha Faki, na aliondoka bila ya kusema wapi anakwenda na lini atarudi. Kabla ya kuondoka, alikuja kumwaga Doto na kumsabilia chochote atakacho na kumpa ruhusa ya kwenda atakapo. Faki aliondoka na kwenda na safari zake. Doto alisalia, na kucheza kidege kama atakavyo, na mambo yalifurutu alipokuwa mumewe hayupo. Nyumba yake ilikuwa kama mkahawa, kila atakaye alikuwa na fursa ya kuja na kufanya atakavyo…

*Kurwa na Doto na Muhammad S. Farsy (uk37–38), 1976*

– Kuna ujumbe gani unaojaribu kutolewa na mwandishi katika dondoo hili?

– Je, mwandishi ameweza kuuwasilisha ujumbe wake kwa ufasaha na kuvutia? Jadili.

– Toa mawazo yako kuhusiana na matatizo anayoyajadili mwandishi hasa ukiyahusisha na matatizo ya ndoa siku hizi.

**1.** (b)

**Siumwi Mara ya Pili**

Sikhiofii kutukanwa, nakhofia kutukana
Vitabuni imenenwa, watu hupata laana
Madhambi mengi huvunwa, kwa ringo na kujiona
Siwezi kuramba tena, sumu nal'okoswa nayo

Sumu nal'okoswa nayo, nendaje kuramba tena?
Nifishwapo nayo hiyo, vipi nitaonekana!
Kwa hiyo siku ambayo, wazishi watakutana?
Kwa hiyo sirambi tena, sumu nal'okoswa nayo

Miba nal'otonwa mwando, ngozi yangu ikachana
Ikanitia uvundo, hatibiwa n'kapona
Siiwekei upendo, mshawasha nayo sina
Mimi siyendei tena, sumu nal'okoswa nayo

Shimo al'ongiya nyoka, dhahiri siyo kwa dhana
Yuangia na kutoka, mwenzangu kagongwa sana
Katu sitajipeleka, kwa nguvu tutagombana
Kamwe sitaramnba tena, sumu nal'okoswa nayo

Tendo lile la awali, tunguze hazitapona
Ungaomba tafadhali, chombezo kila aina
Ninaswe mara ya pili, hola! Sitapatikana
Elewa sirambi tena, sumu nal'okoswa nayo

*Amiri A. S. Andanenga (Sauti ya Kiza), Jua, Juzuu ya Pili/Na.7, Novemba/Disemba, 1998*

– Shairi hili lina ujumbe gani?

– Mshairi anatumia mbinu gani kuwasilishia ujumbe wake?

– Vipi picha zilizochorwa na mshairi zinahusiana na matatizo anayojishughulisha nayo katika shairi lake?

– Mshairi anazungumza na nani katika shairi hili? Toa ushahidi.

## SEHEMU B

*Andika insha moja kutokana na vichwa vifwatavyo. Insha yako ihusu angalau kazi mbili za sehemu ya tatu ulizozisoma. Mapitio ya kazi nyengine yanaruhusiwa, lakini yasiwe msingi wa jibu lako.*

**Wanawake**

**2.** *Ama*

(a) Kwa kurejelea kazi mbili ulizosoma katika sehemu hizi onyesha jinsi waandishi wawili wanavyofanana au/na kutofautiana katika kumtazama mwanamke katika kazi zao.

*Au*

(b) Jadili vipi **jinsia** ya mwaandishi imeathiri masuala ya wanawake kama yanavyojadiliwa katika angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii.

**Riwaya na Jamii**

**3.** *Ama*

(a) Chagua kazi angalau mbili katika sehemu hii ujadili na kuonyesha jinsi ***wahusika*** wake wanavyoyakabili matatizo ya kijamii yanayozungumziwa katika kazi hizo.

*Au*

(b) Kwa kurejea angalau kazi mbili za sehemu hizi, jadili vipi mabadiliko ya kisiasa na kijamii yanavyojitokeza katika kazi hizo.

**Tamthilia Linganishi**

**4.** *Ama*

(a) "Wanatamthilia wa kisasa wanayatazamna matatizo ya jamii katika mtazamo wa ndani badala wa nje." Ijadili kauli hii huku ukirejelea angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii.

*Au*

(b) "Baadhi ya tamthilia zilizomo katika sehemu hii zinaonyesha waziwazi hamu ya waandishi wake kutumia ***vipengele vya kifasihi simulizi*** kujengea tamthilia zao kifani na kimaana." Lijadili wazo hili ukitoa mifano kutokana na angalau mbili ya tamthilia ulizosoma katika katika sehemu hii.

**Kipengele cha Utaifa**

**5.** *Ama*

(a) Chagua kazi mbili kulinganisha matatizo ya kitaifa ya zamani na sasa kama yanavyojitokeza na kujadiliwa katika kazi hizo.

*Au*

(b) Jadili vipi ***anuwani*** (*majina*) ya kazi mbili ulizozisoma katika sehemu hii yanavyoshikamana na matatizo yanayosimuliwa katika kazi hizo.

**Mabadiliko na Upya katika Fasihi ya Kiswahili**

**6.** *Ama*

(a) Chagua kazi mbili katika sehemu hii na uonyeshe vipi ***maudhui*** yake yalivyo ya kisasa.

*Au*

(b) Kwa kurejelea angalau kazi mbili, onyesha jinsi ***mbinu ya uchoraji wahusika*** inavyotofautiana baina ya waandishi wawili. Je, unafikiri kwa nini?

**Utanzu wa Riwaya ya Upelelezi**

**7.** *Ama*

(a) Jadili kipengele cha ***taharuki*** kilivyojengwa katika angalau riwaya mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii.

*Au*

(b) Fananisha na kutofautisha kipengele cha ***ujengaji wa mtiririko wa visa*** *(ploti)* katika angalau riwaya mbili ulizozisoma katika sehemu hii.